**Learning by Ear 2011 – Road Safety**

**Episode 06 – Enforcing Safety Measures**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Martin Vogl**

**CHARACTERS:**

Onyesho la 1:

- PAMELA (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 30-40)
- GRACE (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 70-80)

Onyesho la 2:

- GRACE (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 70-80)
- ABIRIA 1 (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 20-30)
- ABIRIA 2 (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 30-40)
- KIKUNDI CHA ABIRIA

Onyesho la 3:

- GRACE (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 70-80)
- PETER (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 60-70)
- DEREVA WA BASI (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 40-50)
- MWENYE BASI (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 30-40)

- KIKUNDI CHA ABIRIA
- Intro/Studio/Outro:
- MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)
- GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI (MWANAMUME)

**Intro:**

**0. Beatrice:** Karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha yako na mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani. Jina langu ni Beatrice.Kwenye vipindi vyetu vyote kumi tunaandamana na familia ya Wanjiru. Tunaangazia maisha yao ambapo walishuhudia maafa yanayotokana na ukosefu wa usalama barabarani barani Afrika. Tunazungumza pia na mtaalamu wa usalama barabarani ili tujue jinsi ya kuhakikisha usalama zaidi barabarani kwa lengo la kuokoa maisha. Katika kipindi kilichopita Samuel alielewa umuhimu wa kutunza gari lake baada ya ajali aliyopata kutokana na breki za gari kukwama. Katika kipindi hiki, Grace, ambaye ni mama yake Pamela, anakwenda safari ndefu ya basi kuja mjini kumsaidia binti yake.

## Scene One: On the telephone

**1. PAMELA:** Mama, una hakika unataka kuja mjini? Itakubadi usafiri kwa basi la usiku na ninajua hupendi.

**2. GRACE:** **(on the phone)** Pamela, tayari nimeshakata tikiti na kwa vyovyote vile siwezi kuvunja safari. Naamini safari itakuwa salama. Nitapanda basi mwendo wa saa tatu usiku. Nitalala hadi tutakapofika mjini. Kwani kuna tatizo gani?

**3. PAMELA:** Hakuna, mama. Utafika salama. Pengine nitamtuma Peter aje kukupokea kituoni. Niletee ujumbe wa simu utakapokaribia kufika mjini. Safari njema, mama! Tutaonana kesho!

**4.GRACE:** **(on the phone)** Haya! Tutaonana kesho tukijaliwa! Kwaheri !

## Scene Two: On the bus

**5. SFX Atmo:** **Inside bus humming along**

**6. GRACE:** Kumekucha. Napenda hali ikiwa hivi, baina ya giza na mwangaza… **(she pushes her neighbour)** Safari imekuwa nzuri sana. Nadhani tuko karibu kufika.

**7. PASSENGER 1:** **(half asleep)** Samahani, wasemaje? Naam, tunakaribia mjini. Nadhani tuna kiasi nusu saa hivi….

**8. GRACE:** Imekuwa safari nzuri sana. Nachukia sana safari. Ni nadra kwangu kuondoka kijijini lakini ninakwenda kumtazama binti yangu ambaye alihusika kwenye ajali mbaya… na mjukuu wangu na mkwe wangu pia. Utaamini kwamba wote walipata ajali katika juma moja?

**9. SFX:** **BANG. ENGINE CUTS OUT**

**10. SFX: LOTS OF SCREAMING**

**11. GRACE:** Kuna nini? **(screaming)** Nini kimetendeka!?

**12. SFX: LOTS OF SCREAMING**

**13. PASSENGER 1:** Tushuke kutoka kwenye basi. Ebu inuka twende. Umechukua mkoba wako? Uchukue upesi!

**14. GRACE:** Yule mtu yuko salama? Nadhani amerushwa kutoka kwenye kiti alichokuwa amekalia… Bahati yake angali makini.

**15. PASSENGER 1:** Nani ajuaye pengine amevunjika mkono au kiungo kingine….. Ninatumai tutapata msaada haraka iwezekanavyo. Dereva yu wapi?

**16. GRACE:** Yule pale. Anaonekana ameshtuka sana…

**17. PASSENGER 1:** **(to other passenger)** Samahani lakini, unajua kilichotendeka?

**18. PASSENGER 2:** Nadhani dereva alisinzia akiwa kwenye usukani. Itakuwaje agonge kibao cha usalama barabarani kando ya barabara? Hakuna magari mengi barabarani wakati huu.

**19. PASSENGER 1**: Hajapumzika tangu tulipoanza safari saa saba zilizopita. Hajapumzika hata mara moja .

**20. GRACE:** Mbona?

**21. PASSENGER 2:** Nadhani wewe si mtu wa safari za mara kwa mara. Makampuni ya mabasi hujaribu kupunguza matumizi kwa kuwaajiri madereva wachache. Pengine huyu dereva alikuwa ametoka safari mjini jana kabla ya kuanza hii safari ya kurejea mjini. Hizo ni saa kumi na nne za kuendesha gari mfululizo bila kupumzika. Hakuna mtu anayeweza kufanya kazi hivyo kisha asisinzie.

**22. GRACE:** Kweli? Ni hatia mtu kufanya hivyo. Nitampigia simu binti yangu nimjulishe.Pengine ndio sababu Pamela alikuwa na wasiwasi sana kuhusu safari yangu hii ya basi.

**<u>SCENE THREE: By the side of the road</u>**

**23. SFX Atmo: Cars driving past**

**24. GRACE:** Peter! Peter…Niko hapa!

**25. PETER:** Nishakuona. Nimejitahidi kufika hapa kwa haraka. Pamela ana wasiwasi kama nini… Uko sawa? Nini kimetokea?

**26. GRACE:** Watu wote wanasema dereva alisinzia kisha akagonga kibao cha usalama barabarani.

**27. PETER:** Kama kawaida! Na dereva mwenye yuko wapi? Yuko hapa?

**28. GRACE:** Yule pale pamoja na mwenye basi. Hakuna anayetuarifu kinachoelendelea.

**29. GRACE:** Unakwenda wapi, Peter? Subiri, Peter, tulia!

**30. PETER:** **(angry)** Dereva ni nani… wewe? Una akili timamu wewe kwenda kusinzia ukiwa kwenye usukani? Huoni kwamba unahatarisha maisha ya abiria hawa wote?

**31. BUS DRIVER:** Mimi ni dereva mwenye uzoefu wa kazi. Nadhani mbwa alipita mbele yangu na mimi nikajaribu kumkwepa.

**32. PETER:** Muongo mkubwa! Abiria wote wanasema ulisinzia. Nani mwajiri wako?

**33. BUS OWNER:** Niko hapa. Una shida gani? Hukuwa kwenye basi. Unajuaje yaliyotendeka ?

**34. PETER:** Yule mama pale ni jamaa yangu na alikuwa kwenye basi. Nimekuja kumchukua. Na anasema abiria wote walimwona dereva akisinzia. Mbona unamfanyisha huyu bwana kazi kwa muda wa saa saba bila kupumzika? Nasikia kabla ya safari hii alikuwa amekwenda safari nyingine bila kupumzika.

**35. BUS OWNER:** Hilo ni jambo la kawaida. Hakuna asiyefanya hivyo. Unataraji nitaweza kushindana na makampuni mengine iwapo nitaongeza idadi ya madereva? Hata hivyo amezoea kwenda safari mbili mfululizo …

**36. PETER:** Upumbavu gani huo? Hujali usalama wa abiria wako?

**37. BUS OWNER:** Kwani abiria wana nini? Wote ni salama. Na usianze matusi hapa! **(goes to hit Peter)**

**38. PETER:** Ikiwa unataka vita… **(starts going for the bus owner)**

**39. CROWD:** **(sounds of fight, screams)** Acheni! Tafadhali, Acheni!

**40. GRACE:** Peter, unafanya nini? Acha! Utaishia rumande. Acha, nishakwambia!

**END OF SCENE THREE**

**SHORT MUSIC**

**41. BEATRICE:** Naam, kama ulivyosikia katika kipindi cha sita cha mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani, ni zamu ya Grace, mamake Pamela, kushuhudia ukosefu wa usalama barabarani! Humu studioni tunaungana naye George, mtaalamu wetu wa usalama barabarani. Karibu George!

**42. GEORGE:** Asante.

**43. BEATRICE:** Nadhani tuanze kwa kuwaambia wasikilizaji wetu kwamba si madereva wa mabasi ya safari ndefu tu wanaosinzia wakati wanapoendesha magari. Yeyote, akiendesha gari kwa muda mrefu, bila kupumzika mara kwa mara huishia kusinzia akiwa kwenye usukani.

**44. GEORGE:** Ukweli mtupu, Beatrice. Kuna msemo usemao “kawia ufike” na msemo huu unawafaa sana hao walio na lazima ya kuendesha magari wakiwa wachovu. Tatizo la madereva wa mabasi na malori ni kwamba wanafuata maagizo ya waajiri wao, kwa hivyo hufanya kazi usiku na mchana bila kupumzika.

**45. BEATRICE:** Una maana kwamba dereva wa basi la safari ndefu anaweza kuagizwa aende safari nyingine kwa muda wa saa maalumu?

**46. GEORGE:** Naam. Na hapewi kipindi cha kupumzika katika safari yote nzima. Kwa hivyo dereva ataendelea kusonga na safari bila kusimama wala kupumzika. Ndipo mtu hujipata katika hali iliyompata Grace. Inaonekana kana kwamba dereva alisinzia akiwa kwenye usukani kisha basi likagonga kibao cha barabarani. Katika hali kama hiyo abiria wanaweza kujeruhiwa vibaya au hata kufariki dunia.

**47. BEATRICE:** Tuseme kuna haja ya kuwepo taratibu nzuri za kupishana zamu ili makampuni ya mabasi na malori yahakikishe kuwa madereva wanaendesha magari kwa muda fulani na pia iwe lazima kwao kupumzika?

**48. GEORGE:** Kimsingi ndiyo. Lakini kama ujuavyo barani Afrika, watu hatakosa njia za kuvuruga taratibu hizo. Kusema kweli barabar huwa hatari sana katika vipindi fulani vya mwaka. Wakati wa Krismasi, Pasaka, makampuni hupandisha nauli na kuwafanyisha madereva wao kazi zao. Si jingine ila ni tamaa. Ndiyo, kuna haja ya kuwepo taratibu na usimamizi mzuri ili abiria na madereva wasafiri salama na kuwe na usalama barabarani.

**49. BEATRICE:** Asante, George.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**OUTRO**

**50. BEATRICE:** Katika kipindi kitakachofuata Grace na Peter wanarejeshwa nyumbani kwa pikipiki. Tutasikia wakielezwa umuhimu wa kuvaa kofia ya usalama katika mchezo mwingine wa redio uliotungwa na Victoria Averill. Ukitaka kusikiliza kipindi hiki kwa mara nyingine, basi tazama wavuti wetu www. dw.de/lbe. Asante sana kwa kujiunga nasi na jitahidi kuweka usalama barabani!